**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA**

***Unapojibu tafadhali taja:***
Kumb.Na.HMB/H:10/22

17/12/2025

Wananchi wote
Halmashauri ya Mji,
S.L.P. 219,
**BUNDA.**

**Yah: <u>TANGAZO LA NAFASI 18 ZA KAZI YA MUDA YA KUKUSANYA MAPATO KATIKA VYANZO MBALIMBALI VYA MAPATO HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA.</u>**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda anapenda kuwatangazia wananchi wote nafasi za Ajira ya muda ya kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali vya mapato katika Halmashauri ya Mji wa Bunda.

### 1.0. SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 35.
- Awe Mkazi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda.
- Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- Awe mwaminifu katika kazi.
- Awe mwenye uwezo wa kufanya kazi eneo lolote ndani ya Halmashauri ya Mji wa Bunda.

### 2.0. MAJUKUMU

- Kukusanya na kupokea ada na ushuru katika eneo na chanzo alichopangiwa kwa viwango vilivyoainishwa na Sheria.
- Kuwasilisha makusanyo yote benki kwa wakati kulingana na Sheria ya fedha.
- Kutunza vitendea kazi na taarifa zinazohusu makusanyo.

### 3.0. MAOMBI YA AJIRA YAAMBATISHWE.

- Nakala ya cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha NIDA
- Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea.
- Picha mbili passport za sasa (moja ibandikwe kwenye barua ya maombi ya pili iambatishwe na na barua ya maombi).
- Barua ya Mdhamini pamoja passport mbili.

**4.0 MALIPO**

- Kiwango cha malipo kitaainishwa kwenye mkataba wako wa ajira.

**5.0. JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

- Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji wa Bunda,
288 Barabara ya Halmashauri,
S.L.P 219,
**31582, BUNDA, MARA**

***MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI HAYA NI TAREHE 31/12/2025 SAA 09:30 ALASIRI.***

Limetolewa na :

Juma Haji Juma
**MKURUGENZI,**
**HALMASHAURI Y MJI,**
**BUNDA.**

MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI - BUNDA
S. L. P. 219 BUNDA